



**USAID**  
FROM THE AMERICAN PEOPLE



## TANZANIA

### USIMAMIZI ENDELEU WA MALIASILI

Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Maliasili unafanya kazi kuhifadhi ardhi, wanyama pori, misitu, na rasilimali za maji katika mfumo wa ikolojia wa Lyamba Iya Mfipa katika mkoa wa Rukwa. Mradi huu pia unaimarisha uthabiti wa jamii katika wilaya za Sumbawanga na Nkasi kupitia usimamizi bora wa maliasili.

Ikolojia ya Lyamba Iya Mfipa, yenye baioanuai ya kutosha, inakabiliwa na vitisho vinavyoongezeka kutokana na shughuli zinazoshindania ardhi, kama ufugaji, kilimo cha mazao, madini, na kukata miti kinyume cha sheria. Utitiri wa uwekezaji unaotegemea ardhi pia unatishia maeneo nyeti ya kibaiolojia na vyanzo vya maji ambavyo vinaihudumia jamii. Kwa kuongezea, ukosefu wa utawala bora unazuia ushiriki, sheria, uwajibikaji, na uwazi katika usimamizi wa maliasili, na kuzidisha uharibifu.

Usimamizi Endelevu wa Maliasili utafikia malengo yake kupitia hatua mbalimbali za utatuzi unaozingatia raia ambao unaboresha uwezo wa jamii na mamlaka zao za serikali za mitaa na vijiji katika kusimamia maliasili. Utatuzi ni pamoja na mafunzo, mijadala ya umma na mikutano ya uhamasishaji, majukwaa ya habari, na ziara za masomo ya jamii. Mradi huu unakuza utekelezaji wa sheria na sera zinazojumuisha maliasili na mabadiliko ya tabia nchi kama nyenzo muhimu katika kupata utawala bora na usimamizi endelevu wa maliasili.

## MATARAJIO

- Kuunda na kutekeleza mipango shirikishi ya mipango ya matumizi bora ya ardhi, sheria ndogondogo, michakato na zana zingine za usimamizi wa maliasili.
- Kuboresha uwezo wa jamii kuzisimamia taasisi zilizopewa dhamana ya kusimamia maliasili kuwajibika.
- Kuboresha uwezo wa jamii na mamlaka za serikali za mitaa kusimamia maliasili.
- Kuhakikisha jamii zinajua na kutambua kuhusu ufuatiliaji wa uwajibikaji wa jamii katika usimamizi wa maliasili na mabadiliko ya tabia nchi.

**BAJETI** Dola za Marekani 1.99

### MUDA

March 2020– March 2025

### MAENEO YA MRADI

Mkoa wa Rukwa (Wilaya za Nkasi na Sumbawanga)

### MTEKELEZAJI

Lawyers' Environmental Action Team (LEAT)

### MSHIRIKI

Rukwa Sustainable Development Organization (RUSUDEO)

### MAWASILIANO YA USAID

Jestina Kimbesa

Msimamizi wa Mradi

[jkimbese@usaid.gov](mailto:jkimbese@usaid.gov)

### MAWASILIANO YA LEAT

Hana Lupembe

Mkuu wa Mradi

[info@leat.or.tz](mailto:info@leat.or.tz)

Tovuti: [www.leat.or.tz](http://www.leat.or.tz)

Facebook: @LEATTEAM

Twitter: @InfoLeat

### KWA TAARIFA ZAIDI

Tovuti: [www.usaid.gov/tanzania](http://www.usaid.gov/tanzania)

Facebook: USAID Tanzania

Twitter: @USAIDTanzania